# SHERIA NDOGO YA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA UVUVI KWENYE MIALO YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI YA MWAKA, 2020

TANGAZO LA SERIKALI NA. 182 la tarehe 6/3/2020

TANGAZO LA SERIKALI NA. 182 la tarehe 6/3/2020

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)
(SURA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 89)*

SHERIA NDOGO YA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA UVUVI KWENYE MIAI YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI YA MWAKA, 2020

Jina la sheria na muda wa kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo y Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi kwenye Mialo y Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ya Mwaka, 2020, n itaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti l Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii, itatumika katika eneo lote l Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama itaelekezw vinginevyo-

"*Afisa Mwidhiniwa*" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliw kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"*BMU*" (Beach Management Unit) maana yake ni kikundi ch usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwenye mialo;

"*chombo cha usafiri majini*" maana yake ni mtumbwi w injini, kasi,dau au mashuwa;

"*Halmashauri*" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa y Kinondoni;

"*Kamati*" maana yake ni Kamati ya BMU;

"*Kituo*" maana yake ni eneo maalum lililotengwa kwa ajili y BMU kuendesha shughuli zake na wavuvi kushushi samaki wanapotoka kuvua;

"*Mjumbe*" maana yake Mjumbe wa Kamati ya BMU;

*"Mkurugenzi"* maana yake ni Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni au Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

*"mwalo"* maana yake ni sehemu ya kando kando ya bahari ambayo imetengwa kwa ajili ya shughuli za uvuvi na usimamizi wa BMU katika shughuli za uvuvi;

*"mvuvi halali"* maana yake ni mtu yeyote anayemiliki leseni halali ya shughuli za uvuvi;

*"nyavu"* maana yake ni nyavu za makila (gillnets) zenye macho yenye ukubwa wa nchi 5,6 na kuendelea;

*"ndoano"* maana yake ni ndoano za saizi namba 7,8, 9 na 10 tu zinazoruhusiwa kisheria kuopolea samaki;

*"rasilimali za uvuvi"* maana yake ni mazao yote yatokanayo na shughuli za uvuvi;

*"udhibiti wa ubora wa samaki"* maana yake ni uhakiki na uzingatiaji wa ubora wa samaki, vyombo na vifaa vinavyotumika kuvulia na kubebea samaki kabla ya kwenda viwandani kuchakatwa;

*"Uongozi"* maana yake ni uongozi wa BMU katika mwalo husika;

*"Wakala"* maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha watu, kampuni au shirika ambalo litakuwa limepewa mamlaka na Halmashauri kukusanya ushuru na kusimamia Sheria Ndogo hii kwa niaba ya Halmashauri;

*"zana za uvuvi"* maana yake ni nyavu za makila zenye macho ya ukubwa wa inchi 5, 6 na kuendelea.

ɯmizi wa uli za

4. Shughuli zote zinazofanywa na zinazotokana na rasilimali za uvuvi zilizo katika eneo la Halmashauri zitafanywa chini ya Usimamizi wa Halmashauri.

do wa

5. Kutakuwa na Baraza la BMU ambalo litakuwa na muundo ufuatao:

(1) Kutakuwa na Kamati Tendaji yenye wajumbe kum na tano, wakiwemo Mwenyekiti, Katibu, Mweka hazina, mtunz bohari, mzee maarufu pamoja na wajumbe kumi. Kamati hi itakuwa na jukumu la kusimamia shughuli zote za kikundi.

(2) Kutakuwa na Kamati ya Fedha na mipango ambay itakuwa na wajumbe watano ambao ni Mwenyekiti, Katibu n wajumbe watatu.

(3) Kamati iliyoanzishwa chini ya kifungu kidogo ch (2), itakuwa na wajibu wa kupanga mipango ya kuendesh shughuli za kikundi pamoja na kusaidia kukusanya mapat yatokanayo na shughuli za uvuvi kwa idhini ya Halmashauri

(4) Kutakuwa na Kamati ya doria ambayo itakuwa n wajumbe watano wakiwemo Mwenyekiti na Katibu, itawajibik kufanya doria kwa kusaidia Halmashauri katika utekelezaji w Sheria Ndogo hii.

(5) Kutakuwa na Kamati ya Takwimu na taarif ambayo itakuwa na wajumbe watano wakiwemo Mwenyekiti n Katibu na itakuwa na wajibu wa kukusanya takwimu za maza mbalimbali ya uvuvi kwa kushirkiana na Halmashauri.

Leseni za uvuvi

6.-(1) Mtu yeyote ambaye anajishughulisha na masuala y Uvuvi atatakiwa kuwa na leseni ya uvuvi.

(2) Kila mvuvi atakayesafiri kwenda kuvua nje ya ene lililo chini ya BMU atatakiwa kupewa kibali kwa madhumun hayo.

Usajili wa wavuvi

7. Kutakuwa na orodha ya wavuvi wote katika BM ambapo kila mvuvi atasajiliwa kabla ya kuanza kazi akionyesh kuwa yeye ni mmiliki wa chombo cha uvuvi au ni mwajiriw katika chombo cha uvuvi.

Maegesho ya mitumbwi

8. Mitumbwi yote ya kukusanyia samaki au kusafirish mizigo au abiria itaegeshwa umbali wa mita kumi kutok kwenye uzio.

Kuhudhuria Vikao

9. Kila mvuvi au mwanachama wa BMU atalazimik kuhudhuria vikao vya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wavuv au Kamati ya Mazingira pale vikao vitakapoitishwa na Kamat hizo.

vya

10. Kutakuwa na vyoo vya umma vitakavyo jengwa na kusimamiwa na Halmashauri katika maeneo ya mwalo na vitaendeshwa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Sheria za Afya.

iki wa wa i

11. Magari yote yatakayobeba samaki yatakuwa ni magari maalum yenye kibali cha kusafirisha samaki kutoka kwa Afisa Mfawidhi wa udhibiti wa ubora wa samaki na viwango ambayo yatakuwa na sifa zifuatazo:-

(a) hayatatakiwa kuwa na vumbi au kutu; na
(b) yatatakiwa kuwa na milango iliyotengenezwa kwa kutumia vifaa vinavyo kubalika katika viwango vya ubora.

sa

12. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa iwapo-

(a) atafanya shughuli za uvuvi bila kibali maalum kutoka Halmashauri;
(b) atavua samaki kwa kutumia sumu, mabomu, kemikali au nyavu zisizoruhusiwa au kuvua samaki katika maeneo yasiyoruhusiwa;
(c) atavua samaki kwa kutumia mitego ya mtando (Ring nets) katika maeneo yenye maji madogo chini ya kina cha mita arobaini (40m);
(d) atachafua mazingira kwa kutupa takataka au kujisaidia katika maeneo ya fukwe, bandari au masoko;
(e) atavuna au kukata miti ya mikoko bila kibali maalum;
(f) atajisaidia baharini, mtoni na bwawani au kutotumia vyoo vilivyotengezwa katika maeneo ya makambi;
(g) atavua pweza chini ya uzito wa gramu 500;
(h) atafanya shughuli za uvuvi katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya mazalia ya samaki na viumbe wengine wa baharini,mtoni na mabwawa;
(i) atauza au kukausha samaki katika maeneo machafu, au mchangani;
(j) atauza au kununua samaki katika maji au baharini au sehemu nyingine yeyote isiyotengwa kama soko la samaki;
(k) atamzuia Afisa yeyote wa Halmashauri, au mjumbe wa BMU kutekeleza majukumu yake halali ya usimamizi.

Adhabu

13. Mtu yeyote ambaye atakiuka masharti ya Sheria Ndog hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozw faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miez kumi na mbili au adhabu zote kwa pamoja yaani faini n kifungo.

Kufifilisha kosa

14. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kw kumtoza faini ya kiasi kisichopungua shilingi elfu hamsin endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari yake mwenyewe n kujaza fomu maalum iliyoainishwa kwenye Jedwali la Sheri Ndogo hii.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 14)*

**KUFIFILISHA KOSA**

.................................................wa S. L. P............................. nakiri KWA YANGU MWENYEWE mbele ya..............................................ambaye ni ;enzi wa Halmashauri ya Kinondoni kwamba tarehe......ya ......Mwaka.........nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ............ cha Sheria za Udhibiti na Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi kwenye Mialo za Halmashauri ya ›aa ya Kinondoni za mwaka 2020.

amlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri, niko tayari kulipa kiasi cha shilingi elfu i badala ya kushtakiwa Mahakamani.

IBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA YANGU KWA KADIRI YA UFAHAMU WANGU

ehe............... ya mwezi..............mwaka.......................

........................................................... Saini..............................

ya:

...............................................

...............................................

'a...............................................

...............................................

*Tangazo la Serikali Na. 182 (linaendelea)*

Lakiri ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imebandikwa kwen Sheria Ndogo hii kufuatia azimio lililopitishwa katika kikao cha Baraza Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kilichofanyika tarehe mwezi 12 mwaka 2018 na kushuhudiwa.

Lakiri hiyo ikibandikwa mbele ya:-

ARON T. KAGURUMJU
*Mkurugenzi wa Halmasha*
*Halmashauri ya Kinondo*

L.S

BENJAMINI K. SITT
*Mstahiki Meya wa Halmasha*
*Halmashauri ya Kinondo*

NAKUBALI,

Dodoma
8th Februari, 2020

SELEMANI SAID JAFO (MB
*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawa*
*za Mikoa na Serikali za Mit*